# MFALME MHUBIRI

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha MHUBIRI. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

MHUBIRI.

1.Mhubiri?…………………………………………………………….

2..MHUBIRI ANAPATIKANA VIPI?……………………………

3.Kazi…………………………………………………………………….

4.Hekima ………………… ………………………………………….

5. Mwalimu…………………………………………………………

6. Elimu……………………………………………………………….

7. Utajiri……………………………………………………………….

8.Kuokoka…………………………………………………………….

9. Mwisho…………………………………………………………….

# 1. MHUBIRI

"Mhubiri" ni jina la mfalme aliyetawala ktk mji wa Jerusalemu lenye tafsiri ya " Mshauri".

**Mhubiri 1** "Maneno ya **Mhubiri** mwana wa Daudi,mfalme katika Yerusalemu. "

Huyu ni mfalme aliyepewa hekima na mungu na alitunga mithali ambaye vitabu vyake havikuandikwa aliyetangulia baada ya mfalme sulemani kama Mungu alivyomwambia baada ya wewe hatatokea mfalme mwenye hekima kama wewe walitokea wafalme wenye hekima ktk nchi ya Israeli Mfalme mhubiri ni miongoni mwao.

**Mith .9 "**Walakini, kwa sababu huyo Mhubiri alikuwa na **hekima,** aliendelea kuwafundisha watu maarifa, naam, akatafakari, akatafutatafuta, akatunga **mithali** nyingi. "

**Je mfalme Mhubiri ni mfalme Sulemani?**

Kwa hoja ya majina yao unaweza kusema hawa ni wafalme wawili tofauti waliowahi kutawala Israeli. Maana yake hii **mfalme Mhubiri** si **mfalme Sulemani** maana majina yanatofautiana.**Mhubiri** si **Sulemani**

**1Wafalme 1:39** "Na Sadoki, kuhani, akatwaa ile pembe ya mafuta katika Hema, akamtia Sulemani mafuta. Nao wakapiga panda; na watu wote wakasema, **Mfalme Sulemani** na aishi! "

**Mhubiri 1** "Maneno ya **Mhubiri** mwana wa Daudi,mfalme katika Yerusalemu." Kwa habari ya hekima unaweza sema mfalme Sulemani ni Mfalme Mhubiri tafakari,**1Wafalme 3: 12** Huyu ni mungu anamwambia **mfalme sulemani** amempa **hekima** ambayo hatampa mfalme au mtu yeyote baada yake na **Mhubiri 1:16** huyu ni **mhubiri** mwenyewe sio mungu anasema amejipatia hekima kupita waliomtangulia.

## 2.MHUBIRI ANAPATIKANA VIPI?

Mfalme mhubiri kama alivyopatikana mfalme sulemani kwa kupakwa mafuta ya pembe na kuhani Sadoki naye vivyo hiyo. Ukweli wafalme wa Israeli walipakwa mafuta ya pembe walisikwa rasmi kuwa watawala na baadhi ya walipewa roho mtakatifu kisha karama. Mfano Sulemani mfalme baada ya kupakwa mafuta ya pembe Mungu baadaye alimpa Hekima, Sauli mfalme baada kupakwa mafuta ya pembe alitabiri naamini alipewa sehemu kidogo ya roho ya unabii na Daudi mfalme alipopakwa mafuta alipewa roho mtakatifu aliyempa zaburi na roho kidogo ya unabii.

**1wafalme1: 34—39**

"kisha Sadoki, kuhani, na Nathani, nabii, na wamtie mafuta huko, awe mfalme juu ya Israeli; kapigeni panda, mkaseme, Mfalme Sulemani na aishi!

Na Sadoki, kuhani, akatwaa ile pembe ya mafuta katika Hema, akamtia Sulemani mafuta. Nao wakapiga panda; na watu wote wakasema, Mfalme Sulemani na aishi! "

Kwa habari ya mhubiri mfalme inawezekana alipotiwa mafuta awe mfalme wa Jerusalemu alipewa Roho mtakatifu aliyempa hekima au alikutana na mungu aliyempa hekima.au alipata hekima kwa kusoma vitabu vya hekima vilivyoandikwa na Sulemani na kuyatenda aliyojifunza kwa sababu ndiye aliyemtangulia pia kusoma vitabu vingine vya wenye hekima.

Ukweli iko hekima aipatayo mtu kwa kuyatenda yale anayojifunza kutoka ktk vitabu vya wenye hekima ya mungu au mafundisho ya watumishi waliopewa hekima na mungu.

Hekima hiyo ni ya mungu tena safi ukiitenda hukukirimia moyo safi ambao hukupelekea kumwona mungu au kukutanisha Mungu.

# 3.KAZI

Kazi alizofanya mfalme mhubiri wa Jerusalem ktk maisha yake miaka kabla ya kuzaliwa masihi Yesu aliye jibu la kifo yaani ni pekee alitatua tatizo la kifo ni:=>

- Kutawala nchi ya Israeli Mfano **Mhubiri 2: 8**

**Mhubiri 1:12**

"Mimi, Mhubiri, nalikuwa Mfalme wa Israeli katika Yerusalemu. "

- Kufundisha watu wa Israeli maarifa yaani wamjue mungu wa Israeli.

**Mhubiri 12:9**

"Walakini, kwa sababu huyo **Mhubiri** alikuwa na **hekima**, aliendelea **kuwafundisha** watu **maarifa**, naam, akatafakari, akatafuta-tafuta, akatunga mithali nyingi. "

- Kujenga nyumba yake

**Mhubiri 2:4**

"Nikajifanyizia kazi zilizo kubwa; nikajijengea nyumba; "

- Kulima Zabibu na Matunda.

**Mhubiri 2:4-6**

"Nikajifanyizia kazi zilizo kubwa; ….; nikajipandia mashamba ya mizabibu; nikajifanyizia bustani na viunga, na kuipanda humo miti yenye matunda ya kila namna; nikajifanyizia birika za maji, ya kuunyweshea mwitu mlimopandwa miti michanga. "

- Kufuga kondoo na Ng'ombe

**Mhubiri 2:7**

," …... nikawa na mali nyingi za ng'ombe na kondoo,…….; "

# 4. HEKIMA

Mfalme Mhubiri wa ktk kitabu cha Mhubiri cha Agano la kale ktk biblia alikuwa na **Hekima peke yake** kama Mfalme Sulemani ..

**Mhubiri 12:9**

"Walakini, kwa sababu huyo **Mhubiri** alikuwa na **hekima**, aliendelea **kuwafundisha** watu **maarifa**, naam, akatafakari, akatafuta-tafuta, akatunga mithali nyingi. "

Ukweli mfalme mhubiri alifahamu nani anayewapa watu Hekima bila hata yeye hekima yake aliyokuwa nayo aliipata kwa Mungu.

**Mhubiri 2:26**

"Kwa sababu **Mungu humpa yeye** aliyemridhia **hekima** na maarifa na furaha; bali mkosaji humpa taabu, ili kukusanya na kututa, apate kumpa huyo ambaye Mungu amridhia. Hayo nayo ni ubatili na kujilisha upepo. "

Kama nilivyotangulia kukuandikia Mfalme mhubiri wa Israeli inawezekana alipewa hekima na Mungu baada ya kutiwa mafuta ya pembe awe mfalme wa Israeli na kujazwa roho takatifu ya Mungu iliyompa hekima au kwa kumuomba mungu hekima,kwa kusoma vitabu vya wenye hekima kama mfalme Sulemani na kujizoeza kutenda aliyojifunza au kwa kutokewa na mungu kama mfalme Sulemani na kupewa hiyo Hekima.

Mfalme mhubiri alitumia Hekima aliyopewa na Mungu kufundisha waisraeli maarifa ili wasiangamie bali Mfalme sulemani alitumia hekima aliyopewa na Mungu **kuhukumu waisraeli**,**kupambanua mema na mabaya.**

**1 wafalme 3 :9** "Kwa hiyo nipe mimi mtumwa wako moyo wa adili **niwahukumu** watu wako, na **kupambanua mema na mabaya**; maana ni nani awezaye kuwahukumu hawa watu wako walio wengi? "

## 4. ELIMU

Kazi alizozifanya Mhubiri nilizoziandika kama kujenga nyumba,kufuga ngombe na kondoo,kulima zabibu na Matunda,kukusanya fedha na Dhahabu(Taxition).kwa wakati wetu zinahitaji Elimu ya kibinadamu ya ujuzi au taaluma ndio mtu hufanya hizo kazi vizuri na kupata matunda mazuri.

Mfalme Mhubiri kwa wakati wetu angelihesabiwa na watu wenye Elimu ya kibinadamu wenye ujuzi au Taaluma kwa kuwa alikuwa mfalme nafasi ya kupata Elimu ya kibinadamu yenye ujuzi au taaluma ilikuwa kubwa tofauti na maskini au wale aliowatawala wenye hali ya kawaida au ya chini (duni).

Kama Mungu akikupa hekima peke yake baada ya kuokoka  kwa ajili watu wake uwafundishe maarifa yaani Kanisa una kibali mbele za mungu cha kwenda kujifunza elimu ya ujuzi ya ujenzi wa nyumba(House builder,Civil engineer),Elimu ya kilimo(fruit production,livestock keeping), Elimu ya ukusanyaji mapato au  kodi.(Taxition) ukianzia ngazi ya cheti (certificate) , stashahada (Diploma) hadi Shahada (degree).

Ni Elimu ya Kilimo  ukijifunza kufuga ng'ombe na Kondoo inaweza kukufanya kuwa na mali nyingi za kondoo na Ng'ombe na kuwa Tajiri kama Mfalme mhubiri ukijifunza kumtolea mungu kwa hekima wala si kwa upumbavu.Ijapokuwa kazi zote nilizoziandika alizozifanya mfalme mhubiri zinaweza kukufikisha kwenye Utajiri ukipewa hekima na mungu itumie kwa ajili ya mungu. Kusoma elimu ya kibinadamu ni muhimu kwako.

## 5. MWALIMU

**Mhubiri 12:9**

“Walakini, kwa sababu huyo **Mhubiri** alikuwa na **hekima**, aliendelea **kuwafundisha** watu **maarifa**, naam, akatafakari, akatafuta-tafuta, akatunga mithali nyingi. “

Kwa wakati wetu Hekima hupatikana kwa kuokoka ,Mungu akikupa hekima pengine na kunena kwa lugha  na Yesu akikupa **huduma ya ualimu wa maarifa** ya Mungu ufundishe kanisa lake unafanana na mfalme mhubiri kwa hiyo kazi ya kufundisha watu wa mungu maarifa.

Kwa leo tunaweza sema huduma ya ualimu wa maarifa ya kufundisha watu wa mungu yaani Israeli ilikuwa ndani ya Mfalme Mhubiri.

Mfalme Mhubiri tunamwita ni mwalimu kwa sababu ya kazi yake ya kufundisha watu wa Israeli maarifa kama Yesu walivyomwita Rabi yaani mwalimu kutokana kazi yake ya Kufundisha watu ufalme wa mbinguni.

**Mathayo 4.23** “Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, **akifundisha** katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu. “

Tofauti ya mwalimu Mfalme Mhubiri na Rabi Yesu ipo kwenye uweza au karama zingine.Kwa wakati wetu na kanisa tungelisema mfalme Mhubiri alikuwa na karama moja tu yaani Hekima lakini Yesu kama masihi alikuwa na zote mfano Hekima na miujiza.

Ukiwa umepewa hekima na kunena kwa lugha peke yake unaweza kukitumia kitabu cha Mhubiri kufundisha kanisa maarifa mbali na vitabu vingine ktk biblia

## 7. UTAJIRI

Mfalme Mhubiri alikuwa **Tajiri** kwa sababu alikuwa na mali nyingi za kondoo na ng'ombe kumbuka alikuwa na **Hekima** kadhalika na Mfalme Sulemani alipewa **Hekima** na **Utajiri** pia.

**1 Wafalme 3:11 –13**

"Mungu akamwambia, Kwa kuwa umeomba neno hili, wala hukujitakia maisha ya siku nyingi; wala hukutaka **utajiri** kwa nafsi yako; wala hukutaka roho za adui zako; bali umejitakia akili za kujua kuhukumu; basi, tazama, nimefanya kama ulivyosema. Tazama, nimekupa moyo wa **hekima** na wa akili; hata kabla yako hapakuwa na mtu kama wewe, wala baada yako hatainuka mtu kama wewe. Na mambo yale usiyoyaomba nimekupa, mali na fahari, hata hapatakuwa na mtu katika wafalme kama wewe, siku zako zote. "

**Mhubiri 2:7**

"Nami nikanunua watumwa na wajakazi, nikawa na wazalia nyumbani mwangu; tena nikawa na **mali nyingi za ng'ombe** na **kondoo,** kupita wote walionitangulia katika Yerusalemu; "

Ukipewa Hekima peke yake labda na kunena kwa Lugha na Mungu,Yesu au Roho mtakatifu baada ya kuokoka na kujazwa Roho mtakatifu una kibali mbele za Mungu cha kuwa tajiri wa mambo ya mwilini na rohoni pia ktk Bwana Yesu.

Mfalme Mhubiri na sulemani walikuwa na hekima na kuwa majiri wa mwilini na sehemu fulani ktk roho kadhalika Yesu na Paulo mtume walikuwa na hekima na walikuwa matajiri wa siri za Mungu ktk roho, Mojawapo ya kazi ya hekima ni kukufanikisha. Hekima ya mungu humfanisha yule aliye nayo kuwa tajiri kwa njia ya haki. Kwa njia ya hekima yamungu nguvu za utajiri kutoka kwa mungu hudhihirika ktk shughuli za kazi ya mikono yako.

# 8. WOKOVU

Wokovu wa mtumishi wa Yesu anayefanana na Mfalme mhubiri lazima ushike na kutenda mambo yafuatayo yaliyoayomo ktk biblia takatifu:=>

- Amri za Mungu na Yesu

Kushika na kuzitenda amri za mungu na Yesu ni lazima ukivunja usipotubu laana iko inakuatilia au fimbo ya Yesu kwa u mtoto mbele za Baba yake Yesu.

- Kufundisha kanisa maarifa ya Mungu

Kufundisha kwako ni kazi mbali na kuwa huduma kumbuka Mungu aliwaambia waisraeli wafanye kazi siku sita na ya saba ni ya Bwana ni sabato wasifanye kazi.Kufundisha kama kazi unatakiwa kutimiliza huduma yako kila upatapo kibali kwa Bwana Yesu.

- Mche Mungu

Kumcha mungu ni kuchukia uovu kama kiburi , majivuno na njia mbovu au mbaya .Huko kunatunza upako ulio juu yako.

- Maisha ya Toba

Ukimkosea mungu mfano kuvunja amri zake labda hujashika sabato kimbilia toba. Tubu kosa lako na usilirudie.

- Kutenda mema anzia kanisa

Uwe mwema kwa watu wa kanisani kwako akopaye kwako mfadhili msimpe kisogo uwe mkweli kama huna mwambie sina .

- Yale mema unayowafundisha wengine nawe uyatendee kazi.

Hayo mambo ya muhimu ktk wokovu wa mtumishi wa Yesu anayefanana na Mfalme mhubiri ambayo ukiyashika na kuyatenda mungu anakupenda. Ukimwomba lolote lililo sawa na mapenzi yake anakupa kufumba na kufumbua kwa kuwa unayashika ya kwake na kuyatenda.

# 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**

Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :

**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 9332

**MWENGE— DAR-ES-SALAAM TANZANIA**



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034